

SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO)



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

JUMATATU, 28 NOVEMBA, 2022.

JITIHADA ZILIZOFANYIKA ZA KUKABILIANA NA HALI YA UPUNGUFU WA UMEME

Mnamo siku ya Jumatano, tarehe 23 Novemba 2022, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lilitoa taarifa ya hali ya upungufu wa umeme pamoja na kueleza jitihada za muda mfupi, wa kati na mrefu zilizopangwa kuchukuliwa ili kukabiliana na kadhia hii.

Leo Jumatatu, 28 Novemba 2022, Shirika linatoa taarifa ya jitihada za muda mfupi na za muda wa kati zilizochukuliwa katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa umeme kama ifuatavyo;

JITIHADA ZA MUDA MFUPI ZILIZOFANYIKA

Zifuatazo ni jitihada za muda mfupi zilizofanyika ili kuingiza jumla ya megawati 90;

- Tayari tumeshakamilisha matengenezo ya mtambo mmoja wa LM6000 katika kituo cha Ubungo namba III. Aidha, tayari mtambo huu umeshaanza kuingiza megawati 35 za umeme katika Gridi ya Taifa kuanzia tarehe 25 Novemba 2022 kama tulivyoeleza hapo awali;
- Matengenezo ya mtambo mmoja wa kituo cha Kidatu yapo katika hatua za mwisho kukamilika. Na tunatarajia mtambo huu utaanza kuingiza megawati 50 za umeme katika Gridi ya Taifa ifikapo tarehe 30 Novemba 2022 kama tulivyoeleza hapo awali;
- Matengenezo katika kituo cha Kinyerezi namba II yamekamilika na kituo kinazalisha umeme katika na uwezo wake;
- Majaribio ya mitambo miwili katika kituo cha upanuzi cha Kinyerezi namba I yanaendelea, na kwa sasa mitambo hii inaingiza jumla ya megawati 65 za umeme katika Gridi ya Taifa. Na tunategemea hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Disemba 2022, mitambo hii itakuwa inazalisha jumla ya megawati 90 kama tulivyoeleza hapo awali;
- Bado tunaendelea na kazi za matengenezo ya mitambo miwili ya Ubungo namba III ambapo baada ya kukamilika mwishoni mwa Disemba 2022, itazalisha jumla ya megawati 40 za umeme.

JITIHADA ZA MUDA WA KATI ZILIZOFANYIKA

- Tunategemea mitambo mingine miwili kuanza kufanya kazi katika kituo cha upanuzi cha Kinyerezi namba I kuanzia mwezi Februari 2023 ili kuingiza megawati 90 za umeme katika Gridi ya Taifa.

Iwapo mvua zitaendelea kunyesha katika mabwawa yote ya kufua umeme na matengenezo yaliyobakia kukamilika kama yalivyopangwa, basi tunategemea hali ya umeme itaendelea kuimarika na hivyo tunatarajia kiasi cha upungufu wa umeme kwa siku kuendelea kupungua kutoka wastani wa kati ya megawati 300 hadi 350 wiki iliyopita hadi kufikia megawati 100 za umeme wiki hii.

Wakati kazi zote hizi zikiendelea kufanyika, Shirika litaendelea kutoa taarifa ya hali ya umeme na ratiba ya upungufu wa umeme kadri inavyozidi kuimarika kupitia kutoa taarifa kwa vyombo vya habari, mikutano na maandishi wa habari, mikutano na wadau katika mitandao (twitter space na club house), tovuti yetu ya www.tanESCO.co.tz, kwenye magroup ya whatsapp ya wateja, magazeti na kwa kuwatumia ujumbe mfupi wa maneno (SMS) wateja wetu.

**IMETOLEWA NA;
KURUGENZI YA MAWASILIANO NA UHUSIANO KWA UMMA,
TANESCO - MAKAO MAKUU.**